# KISTE EXAMINATION PANEL
# BENCHMARK {006}
## DARASA LA NANE – KISWAHILI: LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambaco si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kujaliza visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile nmba tatu za mwisho za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.

    **Kwa mfano:**
    **Katika Kijitabu cha maswali**

    **17.** Mbwa mdogo sana ni
    A. Kimbwa
    B. Jibwa
    C. Kijibwa
    D. Jimbwa

    Jibu sahihi ni **C**

    **Katika karatasi ya majibu**

    **16. [A] [B] [C] [D]** **17. [A] [B] [C] [D]** **18. [A] [B] [C] [D]** **19. [A] [B] [C] [D]**

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya maswali, swali namba 17 kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa.

11. Jaza kisanduku chako vizuri. Kujaliza kwako kuwe kweusi kama inavyowezekana.
12. Kwa mkila swali jaliza kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ina maswali 50 iliyopigwa chapa**

**FUNGUA UKURASA**

**Jaza mwanya kutoka 1 – 15 kwa kutumia jibu lifaalo zaidi kati ya majibu manne uliyopewa**

Mwalimu ___1___ darasani huwa tayari kumwandaa mwanafunzi kwa ___2___ bashasha, nao ___3___ kwa adabu. Baadaye ni wajibu wa kila mwanafunzi kelewa ___4___. Mwanfunzi yeyote aliye na ___5___ ya kufua dafu maishani hana budi kumtegea sikio mwalimu. La haula! Kuna wanafunzi ___6___. Hawaambiliki hawasemezeki. Huwajia walimu kwa ___7___. ___8___ wanapoadhibiwa, wavyele wao huwakabili walimu kwa ghadhabu za mbogo ___9___! Kumbe ndipo wahenga wakasema mwana wa kuku hafunzwi ___10___.

1. A. aingiapo B. wanapoingia C. akiingia D. akaingia

2. A. masomo B. mustakabali C. mtindo D. mtihani

3. A. huitika B. huitikikiwa C. huitikia D. huitikwa

4. A. anayofunza B. atakayofunza C. anayofunzwa D. atakayofunzwa

5. A. ufahamu B. hamumu C. hamamu D. fahamu

6. A. jeuri B. mjeruhi C. wajeuri D. mjeuri

7. A. maneno ya juu B. meno meupe C. meno ya pembe D.meno makali

8. A. Wao wao B. Hao wao C. Wale wao D. Wao hao

9. A. kiume B. ndume C. dume C. mume

10. A. kuchokopa B. kudona C. kuchakura D. kuwika

Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda nchi yake kiasi ___11___ kutohisi uzito ___12___ katika ___13___ kwa ajili ya taifa ___14___. Katika miaka iliyopita wakati ___15___ mchanga ishara za uzalendo zilidhihirika kote nchini.

11. A. ya B. cha C. la D. za

12. A. yeyote B. yoyote C. lolote D. wowote

13. A. kujitolea B. kujitolesha C. kujotokezea D. kujitoa

14. A. yako B. zako C. lako D. chako

15. A. niliokuwa B. nilipokuwa C. nilivyokuwa D. niliyokuwa

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi**

16. Mwizi mmoja alikamatwa. Tumia sita badala ya mmoja.
   A. Mwizi wa sita alikamatwa.
   B. Wezi sita walikamatwa.
   C. Wezi wasita walikamatwa.
   D. Mwizi msita alikamatwa.
17. Ni neno lipi lenye sauti mwambatano?
   A. Mvua
   B. Liwa
   C. Kunja
   D. Wayo
18. Ni jibu lipi lenye vivumishi pekee?
   A. Gumu, upesi, nadra, langu
   B. Safi, yote, sana, halafu
   C. Laini, nne, kama, mno
   D. Bora, pengine, zile, kwao
19. Ni orodha ipi yenye msamiati wa jikoni pekee?
   A. Uteo, mchi, seredani, dawa
   B. Mchi, uteo, mche, mbuzi
   C. Seredani, kipuli, uteo, mbuzi
   D. Mbuzi, seredani, mchi, uteo
20. Kanusa sentensi hii:
   Kujali kwangu kumenisaidia.
   A. Kutojali kwangu kumenisaidia.
   B. Kutojali kwangu kujanisaidia.
   C. Kutojali kwangu hakujanisaidia
   D. Kujali kwangu hakujanisaidia
21. Damu ni kwa jeraha kama vile _______ ni kwa jipu
   A. usaha
   B. nta
   C. matongo
   D. oga
22. "Ukitaka la waridi sharit udhurika," babu aliniambia, kwa usemi wa taarifa ni
   A. Babu aliniambia kuwa ningetaka la waridi sharti nidhurike
   B. Babu alinishauri kuwa ningetaka la waridi sharti ningedhurika
   C. Babu aliniuliza kuwa ningetaka la waridi sharti ningedhurika
   D. Babu alisema kwamba nikitaka la waridi sharti nidhurike
23. **Andika sentensi hii katika wingi**
   Seremala amemwona mjusi.
   A. Seremala amemwona wajusi.
   B. Maseremala wamewaona mijusi.
   B. Maseremala wamewaona wajusi.
   C. Seremala wamemwona mijusi.
24. Sigi, kipanga, ninga, mwewe ni msamiati wa
   A. hayawani
   B. nyuni
   C. samaki
   D. wadudu
25. Ni orodha ipi iliyo na sauti ghuna pekee?
   A. s, ny, gh, h
   B. v, dh, ny, b
   C. j, gh, th, f
   D. p, ch, ng, n
26. Rangi ya mbingu na mandhari ya bahari ni
   A. kijivu
   B. nili
   C. zari
   D. samawati
27. **Ji imetumikaje katika sentensi hii?**
   Utunzaji wa mazingira unafaa.
   A. Kuunda nomino
   B. Kurejelea nafsi
   C. Kuonyesha ukubwa
   D. kuonyesha mtendaji
28. Sentensi ipi imetumia taswira jozi?
   A. nyumba yake ni pana kama uwanja wa ahera.
   B. Sherehe ilihudhuriwa na wengi si wake si waume.
   C. Tulimsubiri ni kumngojea mgeni mheshimiwa ukumbini
   D. Ali na mkewe wamekuwa jembe na mpini

29. ______________ ni sayari iliyo na pete

A. Zuhura

B. Nirihi

C. Sarteni

D. Utaridi

30. Kupika viazi au mihogo kwa kuchemsha ni

A. kutokosa

B. kutakasa

C. kubanika

D. kukeneka

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 30**

Taifa, jamii au jumuiya isiyowajali wahitaji wake inaelekea kuangamia.Wahitaji ni kina nani na ni kwa nini wanahitaji usaidizi? Wahitaji ni wafuatao; watoto, wakongwe, wagonjwa na wenye ulemavu wa aina yoyote, wanahitaji usaidizi wa watu wote kwa sababu kila mmoja amepita au atapitia hali hiyo katika maisha yake, kwa mfano utoto na ukongwe. Hali zingine zinaweza kutokea bila kutarajiwa na mtu akajipata hapo, kwa mafano ugonjwa au ulemavu.

Watu hao wamezaliwa na jamii wanamojikuta. Hawakujizaa. Jamii hiyo hiyo iliyowazaa ina jukumu la kuwalea.Isitoshe, zaidi ya yote, utu na heshima ya kibinadamu inadai kuwa yeyote anayehitaji kusaidiwa asinyimwe usaidizi. Kwa kweli awe wa kwanza kushughulikiwa hata kabla ya wale wote wanaojiweza.

Lakini je? Hali iko hivyo maishani? Muulize mhitaji yeyote. Utashangaa. Binadamu akiwa na hali yake timamu kimaumbile, kiafya na kiumri, hujisahau. Ni wachache sana wanaowajali wenzao wasiobahatika. Anasahau kuwa uzima wake ni wa muda tu.

Kila mmoja wetu alipitia utotoni. Akalelewa ndipo akafikia utu uzima. Mbona tuwanyanyase watoto? Hali kadhalika, kila siku sote tunasogelea ukongwe kukijalia kuishi kwa muda mrefu. Je, ni kwa nini tuwapuuze na kuwatupa wakongwe?

Watoto ni hazina ya taifa kwa siku za usoni. Nao wazee vile vile ni rasilmali ya jamii. Tumeendelea kutokana na huduma zao na jasho lao. Bado wanazo busara tele na mengi mazuri ya kuturithisha iwapo tutawasikiliza.

Wagonjwa si wasumbufu, na walemavu je? Hao wanahitaji kusaidiwa tu kiasi cha kuwawezesha kuvitumia sawa sawa vile viuno vyao vilivyo vizima. Upofu, uziwi na ububu hata kulemaa miguu na kutotembea, sio kuwa kazi kwisha! Sio ujinga. Hao ni watu wenye hamu kubwa ya kupatiwa nafasi ya kujishughulikia na kutoa mchango wao wa kujenga taifa kulingana na uwezo wao.

Tuwafikirie, tuwajali, tuwasikilize na tuwasaidie na kuwachukulia wenzetu wahitaji kama binadamu yeyote. Washirikishwe kwenye shughuli zote za kijamii bila kubaguliwa. Tukifanya hivyo tutaendelea.

31. Ni akina nani wanastahili kuwajali watu wanaohitaji usaidizi?

A. Watu wote

B. Wananchi

C. Jamii na familia

D. Wenye utu

32. Zimetajwa aina ngapi za hali ya uhitaji?

A. Tano

B. Tatu

C. Nyingi

D. Nne

33. Ni nini kati ya orodha hii si ulemavu?

A. Pumu

B. Uziwi

C. Upofu

D. Kiguru

34. Zitaje hali zile ambazo kila mtu huzipitia

A. Kuzaliwa na kuzeeka

B. Kulemaa

C. Kuugua na kulemaa

D. Kukongoka

35. Ni sababu ngapi zinazofanya jamii iwe na jukumu la kuwatunza wote wanaohitaji?

A. Saba

B. Nne

C. Sita

D. Tatu

36. Kwa nini mhitaji ashughulikiwe hata kabla ya wale watu wengine?

A. Ili asizidi kuteseka

B. Asije akasahaulika

C. Ili apunguze hasira

D. Kwa vile hajiwezi

37. Watoto na wakongwe huwa wanateswa kwa namna gani?

A. Kudhulumiwa na kunyanyaswa

B. Kudhulumiwa na kupuuzwa

C. Kuonewa na kupigwa

D. Kutupwa na kunyanyaswa

38. Kamilisha methali: Uzee si

A. utoto

B. ulema

C. ujinga

D. ugonjwa

39. Ni ipi njia bora zaidi ya kuwasaidia?

A. Kuwapatia pesa na chakula

B. Kuwahurumia na kuwasikitikia

C. Kuwapatia elimu na maarifa

D. Kuwaonea imani sana sana

40. Kutoa mchango wa kujenga taifa ni

A. ushiriki kwenye shughuli za kijamii

B. kutoa pesa kwenye mikutano ya harambee

C. kuwa mwananchi anayejulikana

D. kuwa mzalendo wa kweli kabisa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujubi maswali 41 – 50**

Jioni ya saa moja, nilimshuhudia Mama Lina akinyunyiza jivu kwenye sakafu iliyolowa maji. Jivu lake halikutosha, akaenda kuomba kwa jirani na akarudi na mkebe mzima wa jivu lenye moto. Alinyunyizia mpaka sakavu iliyokuwa imekunywa maji ikakauka.

Mama Lina alikwenda kuvua karatasi mvunguni na kusongeza meza yake iliyolemaa na kucheza "breki dansi" daima. Alisongeza pembeni na kuwatandikia watoto wake pamoja na mgeni wake. Kasu alishangazwa na maisha hayo yalimkodolea macho na kumshurutisha ayaishi. Alianza kula yamini kuwa maisha hayo hatayaweza kamwe. Aliona afadhali kufa kuliko kuhangaika katika dunia. "Utokako taabu na wendako ndiko dhikini kwenyewe," aliwaza.

Nyota yake ya kuzaliwa ilikuwa ikimcheza mchezo asioupenda kabisa. Baada ya kutandikiwa na kabatari kuzimwa, Kazu alijilaza huku mawazo yakimchoma kwa misumari yenye ncha kali. Jambo la kwanza alilowaza ni kwamba baada ya hapo atakwenda wapi? Hangependa kukaa na yule mama kwa muda mrefu kwa sababu ya mzigo wake alioshindwa kuuchukua. Maana alikuwa na watoto shule nzima.

Nyumba ile ilirowa maji paani na ukutani. Chakula chake cha taabu; na mumewe alikuwa mgonjwa sana kwa mnamo miaka saba sasa ni baadhi ya mambo yaliyomfikirisha Kasu. Mama mwenyewe ni mzuri, lakini pamoja na kuwa anasema anaweza kusaidia, je ni kweli kuwa anaweza? Mumewe alikuwa hana pesa za kulazwa hospitalini. Pesa walizozipata walizila kama zilivyokuja. Palikuwa hapana mahali pengine pa jamaa hii ya Mama Lina kutegemea. Kwani ni nani huyo ambaye angependa kutegemewa pasi na kuwa naya yuategemea watu wengine.

"Kwa nini mtu aishi; Lazima mtu kuishi au tunayapenda maisha sisi wenyewe na kuishi kwenyewe hatuwezi?" aliwaza. Alipokuwa katika mawazo hayo usingizi ulimwiba na kumpumzisha mpaka alfajiri alipoamshwa na Mama Lina aliyekuwa akipambana na jiko lake la

makaa. Alikuwa akiandaa la kiamsha kinywa na baadaye kuondoka kwenda katika shughuli za kujitafutia. Kasu na watoto walilalal mpaka asubuhi. Walipoamka walikunywa chai ya mkandaa walioachiwa kwenye kibuyu.

Walipokuwa wakinywa, Kasu alijiuliza, kwa nini watoto wakubwa wa Mama Lina, Malkia na Mariamu hawakuwa wakienda shule. Lakini je, ikiwa baba yao aliyekohoa alipoimimina chai mdomoni mwake hawezi kwenda hospitali sembuse watoto kupata elimu? "Ni lipi la muhimu zaidi?" Kasu alifikiria. "Hawa watoto watakuwa tena kama mimi, nisiye na elimu. Kila niendako naambiwa hapana kazi," akasema na nafsi yake.

41. Ni nani alishuhudia Mama Lina akinyunyizia sakafu jivu?
   A. Mumewe
   B. Mariamu
   C. Kasu
   D. Malkia

42. Kulingana na makala haya, Mama Lina alikuwa akifanya kazi ya
   A. msaragombo
   B. kijungujiko
   C. shokia
   D. sulubu

43. Nahau, "kula yamini" imetumika kumaanisha nini kwenye kifungu hiki?
   A. Faidi mazuri
   B. Pata mabaya
   C. Zumbushwa
   D. Kuapa

44. Wanawe Mama Lina waliotajwa kwa majina kwenye kifungu hiki ni
   A. Kasu na Mariamu
   B. Mariamu na Malkia
   C. Malkia na Kasu
   D. Malkia, Kasu na Mariamu

45. Katika aya ya pili, si kweli kusema kwamba
   A. Kasu alitaka kujinyonga
   B. Kasu aliudhika na maisha yaliyomkabili
   C. Kasu alimburumia mamake Lina
   D. ilikuwa wakati wa usiku

46. Karatasi zilitolewa wapi?
   A. Chini ya kitanda
   B. Kwenye kitanda
   C. Mezani
   D. Chini ya meza

47. Kulingana na makala haya, ni dhahiri sahiri kusema
   A. familia ya Mama Lina ilikuwa ya mabwenyeye
   B. familia ya Mama Lina ilikuwa ya mwinyi
   C. wao walikuwa makabwela
   D. familia ya Mama Lina walikuwa weledi

48. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyomkera Kasu ila
   A. mzigo uliomkabili Mama Lina
   B. ubwenyenye uliokuwa katika familia ya Mama Lina
   C. idadi ya watoto wa Mama Lina
   D. kutosoma kwa wana wakubwa wa Mama Lina

49. Kisawe cha neno kibatari ni
   A. taa za makombe
   B. kandili
   C. kiango
   D. kibaholuli

50. Kichwa kifaacho kwa habari hii ni
   A. Umasikini wenye majuto
   B. Ugonjwa wa kukohoa
   C. Mama Lina
   D. Maisha ya Kasu